

MAHOJIANO NA CHACHAGE SEITHY L. CHACHAGE JUU YA RIWAYA YAKE *MAKUADI WA SOKO HURIA* (2002)

LUTZ DIEGNER

Dibaji

Chachage Seithy L. Chachage aliyezaliwa mwaka 1955 wilayani Njombe ni mmojawapo wa waandishi wakongwe wa riwaya ya Kiswahili. Hadi hii leo amechapisha riwaya nne. Katika mahojiano haya yaliyofanyika tarehe 30 Machi, mwaka 2004, huko Chuo Kikuu cha Dar es Salaam tulitia mkazo zaidi kwenye riwaya yake mpya *Makuadi wa Soko Huria* (2002). Hivi sasa mwandishi ni Profesa na Mkuu wa Idara ya Sosholojia ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Lini na kwa nini ulipata mbegu ya kuandika Makuadi wa Soko Huria?

Hilo ni swali gumu kidogo. Kwa sababu gani? Mimi nimeanza uandishi wa vitabu toka mwaka 1979 nilipokuwa nikisoma. Nilikuwa mwanafunzi wa sosholojia wakati huo, na kila nikiwa na nafasi nilikuwa naandika – nisipokuwa na nafasi, siandiki. Kwa hiyo nimetoa kitabu cha kwanza mwaka 1980, hicho kinaitwa *Sudi ya Yohana*. Nikatoa *Kivuli* mwaka 1984. Kutoka hapo nikapumzika kidogo mpaka mwaka 1990 wakati nilipochapisha riwaya inayoitwa *Almasi za Bandia*. Na kutoka hapo nimekaa, nimeshindwa kuandika kwa muda mrefu sana, mpaka mwaka 1999 nilipoanza kuandika tena. Sasa huu ulikuwa ni mwendelezo wa kuandika kutokana na kazi nilizokuwa nimezifanya hapo nyuma. Mimi ni mwandishi, najua wakati gani umefikia niandike. Kwa hiyo kama kulikuwa na msukumo fulani, sijui. Ni kwamba mimi ni mwandishi, kwamba ilinibidi kuandika. Ndicho kilichonisukuma hicho.

Na pia katika dibaji ya riwaya uliandika kwamba kulikuwa na wakati ulipokuwa umekata tamaa na kuandika tena.

Ehee, nilikata tamaa kwa sababu kuna wakati nilifikia hali ya kudhani kwamba nilikuwa sijui niandike juu ya kitu gani. Hiyo ni moja. Lakini la pili, ilikuwa ni kwamba kutokana na mabadiliko makubwa yanayotokea sasa nchini hapa: vipi mtu uweze kuainisha hayo mambo yanayotokea bila kuonekana kwamba ni mtu ambaye unaegemea upande mmoja au mwingine, lakini uandike kitu ambacho kitaainisha hasahasa haya mabadiliko ya sasa hivi, ambayo wanayaita utandawizi – utandawazi, *sorry*, utandawazi [kicheko].

Lakini watu wengi wanasema ni utandawizi, au siyo?

Hili neno mtu wa kwanza alilolibadili ni mimi. Siku moja nilipokuwa katika semina nikasema ni utandawizi, sio utandawazi huo. Kwa hiyo sasa nikasema “Vipi niainishe haya mabadiliko?” Halafu unajua kwa sababu ni kitu ambacho ni cha dunia nzima, uongeele juu ya Tanzania ama Afrika, lakini uweze kuainisha haya yote hayo.

MAHOJIANO NA CHACHAGE SEITHY L. CHACHAGE

Kwa hiyo kwa muda mrefu nikasema “Ah! Nadhani kuna ugumu.” Labda nifanye utafiti mkubwa sana. Kwa hiyo nilisema inanibidi nikae miaka mingi sana nikijaribu kutafiti kipi ni kipi.

Mara ya kwanza nikafikia uamuzi wa kuandika hiyo riwaya ni mwaka 1996, wakati nilipopewa kazi ya ushauri, *consultancy*, na shirika moja la uvuvi. Nikaenda Rufiji Delta nikiambiwa kwamba nikafanye *environmental impact assessment* ya huo mradi wa ufugaji wa kamba kule. Na ilikuwa ni kazi mbaya, chafu. Nasema hivyo kwa sababu hawa jamaa walitaka sisi tuandike uwongo, lakini mradi uliwaathiri sana watu. Sasa vile nilivyoona mazingira ya kule, kuanzia misitu na kila kitu, halafu watu wenyewe wa kule, ndivyo nikajua nitaanzia riwaya yangu kule Rufiji Delta. Kwa hiyo nilipata ule ushawishi baada ya kuwa Rufiji Delta. Kutoka hapo niliamua kufanya utafiti mpya, kwenye madini huko, na mahali pengine. Kuanzia Mbamba Bay na mahali pote pengine – nilikwenda sehemu zote hizo ambazo zilizomo katika riwaya.

Ulichukua muda gani kuiandika?

Mwaka 1996 nilikuwa nafanya utafiti na kusoma, lakini mwaka 1999 nilianza kuandika. Na nimeanza kuandika wakati ambapo Mwalimu Nyerere alikuwa hospitalini huko London. Ndiyo sababu nime-*dedicate* hicho kitabu kwa kumbukumbu yake, kwa sababu ilibadilisha hasa mwelekeo wa kutizama hizi nchi zetu. Ile iliniathiri sana. Kwa hiyo kuandika nilianza mwaka 1999, lakini kufanya utafiti tokea mwaka 1996. Kwa hiyo utafiti ukawa ni miaka mitatu hivi, halafu kuandika ni kutoka mwaka 1999 mpaka mwaka 2000. Mwaka mmoja.

Umekusudia kumfikia nani na riwaya hiyo?

Kwa ujumla ni wasomaji wa Kiswahili. Ijapo ningependa labda kila mtu akisome. Lakini kwa sababu mimi ni mwandishi wa Kiswahili, nimewalenga wasomaji kwa ujumla, lakini zaidi wasomaji wa Kiswahili.

Kadri unavyojua wasomaji waliipokeaje riwaya yako?

Kwa ujumla imekuwa ni *positive*. Nilipata *review* moja ya mtu anayeitwa Miki Taseni kwenye *Guardian*, hakupenda kitabu hicho. Lakini mimi nilimwelewa kwamba hakukisoma. Na mimi sikumjibu, sikumjibu kabisa, kwa sababu sikuwa na muda, na pia nilichoandika nimeshaandika.

Aliandika review bila kuisoma riwaya yenyewe?

Ukisoma yaliyomo mle ndani, anataka kukosoa hicho kitabu, lakini nilichosema hasemi. Inavyoonekana ilikuwa kwamba aliona hicho kitabu halafu akakasirika. Halafu labda akasoma kurasa kadha wa kadha, akaamua kuandika juu ya kitabu kadri alivyofahamu yeye. Lakini *otherwise* karibu *reviews* zote, kuna moja ya Profesa Shivji katika jarida la Kiswahili la *Mulika*, ni nzuri kabisa. Na nyingine zimekuwa nzuri. Kwa ujumla siwezi nikakwambia, kwa sababu kutoka mwezi wa Oktoba mwaka 2002 mpaka Disemba, ilikuwa nakala mia tatu zilikuwa

zimeshauzwa. Hiyo, kwa vitabu nchini hapa, ni namba kubwa sana. Kwa hiyo nadhani kwa ujumla imepokelewa vizuri ijapo kuna watu ambao wamekasirika.

Na je, kulikuwa na uzinduzi rasmi?

Ulifanyika, ndiyo. Kuna watu waliokasirika kwa sababu hawataki kuitwa makuadi. Hiyo ni kawaida.

Je, kweli kulikuwa na watu waliojaribu kukuzuia kuandika kitabu hicho kama msimulizi anavyosema?

Hapana. Ile ni staili ya kuandika. Ni kutaka kukumbushia tu kwamba kulikuwa na watu waliofanya mambo ambayo hayependwi. Nimetaka kuainisha tu hali hiyo, lakini hakuna mtu aliyenizua. Kwa sababu nilipoanza kuandika riwaya hiyo nilikuwa Capetown, nilikuwa peke yangu kule. Sikuwa Tanzania hapa. Nilikuja kumalizia hapa. Hakuna mtu ambaye alinizua. Miye na huyu mhusika ni tofauti kabisa.

Na mhusika mwingine Janga Mjuba – je, ulimchanganya kidogo na maisha yako?

Hapana. *Actually* majina mengi mle ndani, ingawa sikutaka kusema hivyo, lakini nimeyageuza [majina] ya marafiki zangu. Janga Mjuba anaitwa [...] [*jina limeachwa*]. Ni mwandishi wa habari pia, halafu ni mwandishi wa riwaya. Yeye nilisoma naye *highschool*, na alikuwa mwanafunzi wangu hapa [Chuo Kikuu]. Kwa hiyo nikageuza jina lake. Huyu Faki Kamari ni [...] [*jina limeachwa*] ambaye pia ni mwandishi wa habari. Kwa hiyo wengi nimewageuza, na hata wengine wanafahamu kabisa, nikaamua kutumia majina yao. Hamna ukweli ndani yake lakini basi.

Na wewe mwenyewe je?

Mimi simo. Ni waandishi wa habari, mimi hapa ni profesa, kwa hiyo tofauti kabisa. Kama nilikuwa Rufiji, ni kweli nilikuwa Rufiji, lakini nimefanya *impact assessment*. Na kuna chama cha *JET, Journalists' Environmental Association of Tanzania*, ambao ni waandishi wa habari ambao wanayapigia debe mazingira. Wao walikwenda kule, lakini sio hao niliowataja. Kwa hiyo nilitumia fursa ya kuwa kule, nilitumia waandishi wa habari, kama ndio wahusika wakuu. Miye simo mle ndani.

Na akina Sifuni je?

Wote ni waandishi wa habari.

Riwaya yako inazungumzia watu na matukio halisi ya jamii ya Tanzania. Unawataja kwa mfano wanasiasa Mtikila na Mrema (Chachage 2002: 6) na mwanasheria Profesa Shivji (keshatajwa: 118ff.). Je, katika kuwachora wahusika kama Mooney, Alhaji Said Seif na wengine, uliwafikiria watu wanaoishi au walioishi kweli?

Ni watu ambao wameishi, na waliishi, lakini si wao majina na tabia zao, siyo wao. Kwa upande mwingine nimegeuza matukio yasiwe kama yaliyotokea. Hata yule Mhindi anayekaa kule hotelini, anayekula kule, ambaye zamani alikuwa *Marxist*, halafu akawa mwingine, ni watu ambao wamekuwepo, lakini siyo majina yao.

Na inakuwaje kuhusu mhusika Mooney?

Hilo sitajibu. Lakini *otherwise*, kama ukifungua kwenye *website*, tafuta juu ya Rufiji Delta, na tafuta kulikuwa na *issue* gani – utaipata. Utaona kama kulikuwa na mtu kama huyu ama vipi.

Mbali na kuzingatia matatizo ya jamii ya Tanzania ya miaka ya karibuni, kama ulivyosema unazungumzia pia historia ya nchi hii, hasa ya eneo la Rufiji. Je, ulifanya uchunguzi maalumu kuhusu historia ya eneo hilo?

Nilifanya. Halafu na hata [juu ya historia] ya Songea, kwa Wangoni na watu wengine pia. Yote ni historia. Na baadhi ya majina, akina Zulu Gama, akina Zwangendaba, ni ukweli. Ingawa hawa wajukuu wao sio wa kweli.

Riwaya yako inaweza kusomwa kama handbook ya ukosoaji wa utandawazi unaotawaliwa na siasa ya soko huria. Hivi juzi [mwanzoni mwa mwaka 2004] Rais Mkapa kama mwenyekiti wa Tume ya Utandawazi alitoa ripoti – kwa Kiingereza – inayowataka Watanzania wazingatie upya manufaa ya utandawazi. Unaonaje hoja hii ya Rais?

Mimi nimekuwa natofautiana sana na watu wengi katika suala hili la utandawazi kwa ujumla. Mimi kwa maoni yangu, huu unaoitwa utandawazi ni kitu ambacho kilikuwepo siku zote. *Globalization* ni kitu ambacho kilikuwepo siku zote isipokuwa ni kitu ambacho wanataka kukigeuza kitu ambacho ni kibaya kiwe kizuri. Ubeberu na ukoloni mamboleo ndio utandawazi. Hakuna tofauti yoyote ile. Kwa hiyo sijaona kwamba utandawazi una manufaa.

Mimi kama naamini kwamba kuna kitu kama utandawazi, ni kitu ambacho kinaitwa *globalization from below*. For example, *human rights* ni *global movement*, *women's rights* ni *global movement* – *that's the real globalization*. *Environmental protection* – *that's the real globalization*. Lakini *other globalization* ambayo ni *movement ya capital*, na *communication or whatever* – *these things* zimekuwepo siku zote, *you know?* Lakini *we can talk about human rights* kwamba ni *phenomenon* ambayo imeanza miaka ya 1945, au *peace movement* ni ya miaka sitini na sabini. Lakini hiyo ya *capital* kutoka wakati wa ukoloni, na hiyo ya watu kutoka wakati walipochukua *slaves* mwaka 1441, akina Goncalves – ni kitu hicho hicho. Kwa hiyo utandawazi ni unyonyaji.

Ni ubeberu. Kitu kimoja cha kujiangalia zaidi ni *impact*, kwamba kuna madhara. [Rais] Alikubali kwamba kuna madhara, ingawa anasema tunaweza ku-*accomodate*, na tunaweza kuishi nao kwa kukaribisha vitu fulani. Kwa hiyo miye ninachopinga ni madhara ya utandawazi.

Mwanzoni mwa riwaya mhusika Janga Mjuba anamtania mpenzi wake Sifuni kwa mas'hara ya kiashiki. Katika mfululizo wa hadithi hakuna sehemu nyingine za kiashiki zinazofanana na sehemu hiyo. Unaonaje kutumika kwa sehemu za kiashiki katika riwaya-dhati ya Kiswahili hasa kuhusu upokezi wake na wasomaji?

Sijui. Mwanzoni mwa riwaya inasimuliwa wakati ambapo Mjuba na Sifuni wameshakuwa wapenzi. Lakini wanaanza kuwa wapenzi wakiwa Rufiji, na hiyo inasimuliwa baadaye. Kwa hiyo kama hakuna sehemu nyingi, ni kwa sababu wanakuwa wapenzi mwishoni. Lakini pia kwa mfano huko walipokuwa Nyamisati, usiku huo wanachokozana pale, kuna hali ya kiashiki pale, bwana aliota ndoto ya kiashiki. Kwa hiyo ni maisha ya kawaida kwamba watu – si binadamu? – wanapendana. Kwa hiyo mimi sioni cha ajabu hapa. Sioni cha ajabu kabisa. Sikutumia hilo kwa kutaka kuvutia tu wasomaji, lakini hicho ni kwamba wao ni wapenzi, na wanaongea maongezi ya kawaida.

Na kwa ujumla unaonaje upokezi wa sehemu kama hizo?

Sijui, kwa sababu mimi nimeandika, na wao kama watapokea vibaya, shauri yao. Lakini mimi nimefuatilia mazungumzo ambayo ninayafahamu, ya kawaida kabisa, ya watu wote.

Mada nyingine ni tabia ya ma-expatriates na hasa waajiriwa wa NGOs kutoka nje. Kwa kutumia mhusika Sorrenson unaonesha metamorphosis yake. Mwanzoni ni mwenye kiburi asiyeonesha ufahamu na sensitivity yoyote kuhusu utamaduni mwingine unaomzunguka. Mwishoni ni mtu aliyejifunza mengi, hasa kuchanganyika na watu na kuwasikiliza. Unafikiri tabia ipi ya ma-expatriates inatawala nchini Tanzania leo?

Sijui. Mimi sijawa na *interaction* kubwa sana na *expatriates* katika miaka ya karibuni. Lakini hawa ninaowazungumzia akina Sorrenson ni wachache sana. Wengine wanakuja kama wataalamu, wanajua kila kitu. Huja kuwabadilisha watu. Na kutamka anasema alikuja hapa kwa sababu yeye ni *gender expert*, kwamba Waafrika wana tabia mbaya, wanadharau wake zao, na wanawatendea vibaya – bila kufahamu ni kitu gani. Kulikuwa na mkutano mwaka 1987 huko York. Unakutana na Mwingereza anasema atakwenda Zimbabwe kusaidia wanawake wajikomboe, hiyo ni *arrogance*. Kati yao *arrogance* ni kubwa sana. Ni kubwa sana. Si kusema kwamba hawawezi kubadilika, ni kweli kuna baadhi yao ambao unakuta kwamba *from being so arrogant they finally become humble, saying "you know, we don't understand much about these people"*.

Je, unapoandika unaandika moja kwa moja au kwa mpangilio?

Sijui, maana'ake mimi nabadilishabadilisha. Unaweza ukaanzia mahala fulani, halafu ukasema hapana, unabadilisha. Kwa hiyo sijui maana'ake hadithi zangu zinaanzia kichwani. Siwezi nikadai ninaweka *plot*. Huwa siweki. Sanasana kama nikishafanya utafiti wangu, nimefahamu kitu fulani, najua nitaongea juu ya kitu fulani. Najua kabisa isipokuwa nitaanza kusoma kitu fulani na kusoma kitu fulani, na kitu fulani, na kitu fulani. Lakini nikishaanza kuandika, nd'o hivyo hivyo.

Kwa hivyo huweki sura ya kwanza itakuwa hivi, sura ya pili itakuwa vile, notes ndogondogo...?

Hapana, ina-flow. Halafu baada ya hapo, kama ninabadilisha njiani nabadilisha vitu. Nikiweza nakibadilisha kitu kutoka sehemu fulani na kukipeleka mahali pengine au kukiondoa kabisa au kukiongezea. Na mara nyingi huwa sijui mahala itakapoishia hadithi. Huwa sijui. Zote nimeziandika hivyo.

Katika riwaya yako mara kadhaa msimulizi anazungumza moja kwa moja na msomaji, kipengele ambacho kinaipa riwaya yako sifa ya fasihi simulizi. Aidha, kwa kuziita sura za kwanza na mwisho Kifungua na Kifunga Pazia uliipa riwaya ladha ya mchezo wa kuingiza. Je, umefanya hivyo makusudi ili kurahisisha usomaji wa riwaya ndefu kama hiyo au kwa sababu ulipenda kuchanganya tanzu mbalimbali za kifasihi?

Kwamba nimetumia fasihi simulizi ni kweli, kwa sababu naipenda. Lakini pia kuna kitu ambacho sijui kama umekiona, licha ya *Kifungua Pazia* na *Kifunga Pazia*: ukisoma zile *titles* za kila *chapter*, ni hadithi peke yake. Kama unasoma, kulikuwa na “Biashara ya Kutukuza Yashindikana”, halafu “Akatokea Binti Wenga”, halafu “Alikuwa na Ndugu Huko Rufiji”, halafu... – ukisoma hizo *titles* zote zile, inakuwa ni kama hadithi hivi. Ilikuwa ni *by sheer accident* nikagundua kwamba *titles* zenyewe ni hadithi. Hii ni *influence* ya fasihi simulizi. Hiyo imeniinfluence sana. Kwa sababu kuna usimulizi na usimulizi. Mimi si mtu wa fasihi wala si *critic* wa fasihi, lakini ni kufikiria *the most successful form* mtu aweze akajikuta anahusika pia. Kwa sababu utakuta katika *Almasi za Bandia* pia kuna mahala msimulizi anaposema “*Ewe msomaji mwema!*”. Ni kama *titles* za *chapters* hapa. Kwa hiyo *in a way* kwa kule unaingia moja kwa moja. Lakini katika hii ni kwa sababu anayesimulia ni mwandishi wa habari mmoja yule anayeitwa Fidelis Mvumi Msakapanofu. Yeye ndiye anasimulia. Anasema “*Ewe Msomaji Mwema!*” Maana'ake ni *the first time* naandika *first person*, hii *novel*. Hizi nyingine zilikuwa *third person*.

Na hii ladha ya mchezo wa kuingiza ilijitokeza tu hivyo?

Zamani kabla sijawa naandika riwaya nilikuwa naandika michezo. Ijapo sijachapisha hata moja. Niliandika wakati wa *highschool*. Mmoja kuhusu dada yake Mkwawa [Chifu wa Wahehe] ambaye inasemekana aliongoza majeshi ya Wahehe katika vita na Wamaasai. Halafu niliandika

MAHOJIANO NA CHACHAGE SEITHY L. CHACHAGE

mchezo mwingine kuhusu Mirambo [Mtemi wa Wanyamwezi]. Kwa hiyo zamani niliandika michezo ya kuigiza, halafu pia nilikuwa *actor* zamani nilipokuwa shuleni. Kwa hiyo hiyo [ladha ya mchezo wa kuigiza] siyo *accident*.

Kwa hivyo hii miswada bado ipo?

Sijui, nafikiri bado ipo nyumbani. Sijui kwa sababu mchezo wa mwisho wa kuigiza niliandika mwaka 1979. Kuamua kuandika *novel the first time* ni mwaka 1979 nilipokuwa chuoni nikiwa nasoma. Kutoka mwaka 1977 hadi nilipojiunga na Chuo Kikuu mwaka 1979 nilikuwa nafanya kazi *Tanzania Publishing House*. Lakini huko nyuma nikiwa *highschool* nilikuwa mchoraji, nilikuwa ni *fine artist*, halafu nilikuwa *musician* wa aina fulani. Halafu nilipokuja hapa chuoni nilitarajia nisomee *fine arts* na *music*. Bahati mahitaji ya kitaifa ya nguvu kazi yaliruhusu zaidi *sponsorship* ya serikali katika nyanja fulani kuliko nyingine. Kwa hali hiyo, ilikuwa *either* nifanye *sociology* au *political science*: nikaipenda *sociology* kuliko *political science*. Kwa hiyo nilifikiri 'How do I continue with my art?' bila ku-*jeopardize my studies*. Kwa hiyo nikakuta kwamba *the only alternative* ni kuandika *poetry* kidogo na kujaribu kuandika riwaya. *That was the first attempt ever. Otherwise* nilikuwa ni mtu ambaye amefanya vitu vingine hivyo kwa muda mrefu sana. Kwa hiyo hiyo sehemu ya *fine art* imeshapotea. Sijachora kwa miaka mingi sana. *Music* imeshapotea kabisa kutoka mwanzoni mwa miaka ya themanini hiyo hiyo.

Ulipiga muziki wa aina gani, au ala gani?

Nilikuwa napiga *rhythm guitar*. Niliacha hiyo tayari. *At least* kwa sababu hakuna nafasi kubwa. Hata kama utaacha kuandika leo, kesho utaandika. Nikishaanza kuandika inanibidi nimalize. Nisipomaliza inaniumiza kwa hiyo *the same with art*. Ukishaanza kuchora namna hii, inaweza kuchukua siku nne au kumi, lakini kwenye *novel* – si utaendelea bwana? *I thought it much easier* kwenye *novels* kuliko kwenye sanaa nyingine.

Unaonaje nafasi ya Makuadi wa Soko Huria katika uandishi wako kwa ujumla?

Tofauti ya *Makuadi wa Soko Huria* na riwaya zangu nyingine, *at least Kivuli na Sudi ya Yohana*, ni kwamba hii [*Makuadi wa Soko Huria*] ni *historical novel*. Utakuta ina-*trace* kutoka 1840s mpaka mwaka 1999 au 2000. *The whole history of Tanzania* imesimuliwa katika njia hii. Pia kuna historia ya *Pan-Africanism* na nyinginezo. [Mhusika] Binti Wenga anasimulia kwa mfano: 'Si wakoloni ndio wameunda Watanzania na Watanganyika? Sisi hatukujua habari hiyo. Sisi tulitoka Afrika Kusini...' *Which is true* – si ndiyo bwana? Haikuwapo mipaka. *In a way it is about telling the whole history of Africa* kwa kutumia Tanzania. *That's the main difference*. Kwamba *that is a historical novel*.

Na unaonaje nafasi yake kifani?

Sijui kama nimebadilika kifani. Lakini *for example* kitu ambacho nakitumia sana katika *novels* zangu zote kwa ujumla ni *flashbacks*. Zote. Kwa hiyo *that's something* kwamba imekuwa *consistent*. Kama nimebadilika sijui. *Infact in a way if you ask me "what do you think of your works?" I love most my first novel.* Ndiyo *when you start writing, the first time ever, all the efforts*, mawazo yote na kila kitu na kila unachokifahamu ni mle ndani. Lakini ikija ya pili, siyo kama ya kwanza. Na ya tatu utajaribu kurudi nyuma huko. *You don't come up with something new.* Lakini *the first one is new, new, new.* *Why in a way i'm so full of Sudi ya Yohana* kuliko *my other novels – I don't know why. Whatever the reason*, lakini *some of us thought* kwamba *there was art*, huku nyingine *I don't know*. Pengine ni *crude* wakati mwingine. *I don't know but that's what I get. But in any case, you see, Sudi ya Yohana* inaonyesha enzi za *seventies*, vijiji vya Ujamaa, *whatever happened to the farmers and to the workers – that's it.* Na Kivuli again ina-*depict the rural areas*, kuelezea *what happened in the seventies*, matatizo ya vijiji na kwenda kule. *Almasi za Bandia is a bit off the road*, kwa sababu *for the first time* na-*explore Europe* na Afrika. Maana'ake kwa sababu nilikuwa nasoma Glasgow. *And what I saw among Africans, and how things were there. That is different. Anyway. Kivuli* sijiui, lakini *the only thing that is actually* tofauti na ile nyingine ni kwamba ni *historical novel*. Hata katika hii, lakini ni lazima inakwenda *that way*. Katika *Makuadi wa Soko Huria* kuna *historical characters* kama Nyerere, akina Kambona, akina Makange. *All these are real historical people. That's the main difference.* Kwamba *some of this depicts history in its own way*, machifu, akina Mputa na wenzao walikuwepo. *These are real historical people. Chiefs* walikuwepo.

Swali la mwisho ni kuhusu matarajio yako ya kuandika riwaya nyingine au kazi nyingine ya fasihi?

Sasa hivi najaribu kuandika tena. Sijui nitafikia wapi, lakini nimeshaandika *chapter* moja au mbili *so far*, na *of course* nilikuwa nimecheleweshwa na matakwa ya kuandika makala za *sociology*, lakini *otherwise* nimekuwa naandika riwaya nyingine mpya. Nimeandika *chapter* moja au mbili. Sijui nitafikia wapi. Lakini labda nitamaliza siku moja.

Kwa hiyo lazima tusebiri ukistaafu utaandika riwaya nyingi sana.

Ah, hapana. Sijui, halafu *of course* nitaendelea kuandika, unajua *I'm just re-writing a book on tourism*, halafu kuna *another book* ambayo ninaiandika kuhusu *education: Against the Barbarians at the Gate of Scholarship. This is a new project.* Kwa hiyo nitachelewa kidogo.

Haya. Nashukuru sana.